

# Mwongozo wa Familia wa Kujifunza

Muhtasari wa yale watoto wanastahili kufahamu na kuweza kufanya na njia za familia kuongeza masomo nyumbani.



“Tunaamini familia ni wenzetu. Niwa kwanza na waelimishaji wa watoto wenye nguvu zaidi . Pamoja tutahakikisha mafanikio ya wanafunzi wote.”

- Mrakibu Emmanuel Caulk,  
Shule za umma za kata ya Fayette

## **Kuhusu mwongozo wetu wa kujifunza:**

---

Mwongozo huu unawakilisha baadhi ya vitu muhimu mtoto wako anapaswa kujua na kuweza kufanya kufikia MWISHO wa mwaka wa shule katika usanaa wa lugha ya Kiingereza (ELA) na Hesabu. Malengo ya kujifunza inasaidia familia na walimu kujua lini wanafunzi wanahitaji msaada zaidi na lini wanahitaji changamoto zaidi.

### **Familia zinaweza kufanya nini?**

---

Kuna mengi ya kufanya kumsaidia mtoto wako kujifunza na kusaidia kuwatayarisha kwa maisha yao ya mbeleni. Haya ni mambo machache ambayo yatawasaidia wanafunzi kufanikiwa:

1. Eleza na mtoto wako jinsi masomo yalivyo muhimu kwako. Waeleze elimu inastahili, kwamba ni msingi wa mafanikio.
2. Fanya shule iwe kipaumbele kwa kumpeleka mtoto wako shulenii kwa wakati kila siku. Kwa kufanya hivyo unaonyesha kwamba ni kipaumbele.
3. Shirikiana na shule kujenga kuheshimiana.
4. Himiza kujitegemea; ruhusu watoto wako wafanye makosa na wakubali wajibu wa chaguo lao.
5. Jadiliana na mtoto wako kuhusu nini kinatendeka shulenii.
6. Wasiliana mara kwa mara na walimu wa mtoto wako kuhakikisha mtoto wako anafanya maendeleo kwa mwaka mzima.
7. Hudhuria mikutano ya mzazi-mwalimu na shughuli zingine za shule inapowezekana.
8. Una haki ya kujua jinsi mtoto wako anavyoendelea; usisite kuwasiliana na mwalimu wake kama una maswali.

### **Kuzungumza na Mwalimu wa Mtoto wako**

---

Ni muhimu kuzungumza na mwalimu wa mtoto wako na shule mara kwa mara kuhusu malengo ya mafunzo ya mwanafunzi wako. Hapa kuna mfano wa maswali unayoweza kuuliza:

- Mtoto wangu ana nguvu wapi na ni wapi anahitaji kuboresha?
- Maendeleo ya mtoto wangu yanapimwa vipi katika mwaka mzima?
- Naweza kuona mifano ya kazi za mtoto wangu? Vipi wanafikia ama hawafikii malengo ya masomo?
- Mtoto wangu yuko njiani kufikia malengo ya masomo ya darasa lake? Kama sivyo, kuna misaada gani shule inaweza kutoa? Naweza kufanya nini nyumbani?
- Mtoto wangu yuko kwa ama juu ya matarajio ya masomo? Kama ndivyo, nini kingine shule inaweza kutoa? Naweza kufanya nini nyumbani?
- Umesoma IEP ya mtoto wangu? Ni misaada gani inayonayofanyiwa mtoto wangu?
- Mtoto wangu anajifnuza Kiingereza. Kukua kwa lugha ya mtoto wangu kunasaidiwa vipi shulenii?

## Kuzungumza na Mtoto wako

---

Hii inasikika kama kawaida?

“Shule ilikuwaje leo?”

“Sawa”

“Ulipanya nini?”

“Hakuna”

Hiyo ni sawa, endelea kuuliza!

Wanafunzi ambao wazazi wao wanazungumza nao kuhusu shule hufanya vizuri kimasomo katika shule. Hizi ni baina ya njia za kumhusisha mtoto wako na kusaidia katika mafaniko yao:

- Tenga wakati fulani kila siku kuzungumza na mtotowako kuhusu shule. Uliza mtoto wako ni darasa gani alipendelea zaidi leo. Kwa nini? Ni kitu gani kimoja angeweza kubadilisha kuhusu siku hiyo? Kwa nini?
- Uliza mtoto wako akueleze kitu kimoja walijifunza wamejifunza leo. Ni nini mtoto wako anafikiri inavutia sana? Ni nini inaonekana kuwa ngumu?
- Pitia makaratsa na miradi ambayo mtoto analeta nyumbani kutoka shulen. Uliza mtoto wako akueleze inaonyesha mafunzo gani?
- Sifia mtoto wako kwa kazi ngumu na juhud, sio wakati tu “majibu ni sahihi”.
- Uliza maswali kuhusu mtoto wako anawaza nini? Unafikiri nini? Unatambua nini? Uliifanya hivyo kwa nini? Kuna njia nyingine ya kupata jibu hilo?

## Kusaidia mafunzo mbali na shule

---

Mafunzo hayapaswi kusimama wakati wanafunzi wanaache shule. Wanafunzi hutumia mda mwingu nje ya shule kuliko katika shule. Hizi ni baina ya njia ambazo unaweza kusaidia masomo nje ya shule:

- Somea mtoto wako, soma na mtoto wako, na uhimize mda wa familia kusoma pamoja — katika lugha unayoipendelea.
- Tenga wakati mtulivu na mahali starehe kwa mwanafunzi wako kufanya kazi za shule za nyumbani ama shughuli zingine za masomo.
- Jaribu kutengeneza ratiba ya kawaida ya kufanya kazi za shule za nyumbani na shughuli zingine za masomo.
- Tumia muongozo huu kwa malengo machache ya masomo; jaribu mapendekezo kadhaa ya masomo ya nyumbani.
- Himiza mtoto wako kutumia ubishi wenye maana kutetea maoni yao. Kwa mfano, kama mtoto wako anataka nyongeza ya mapato, muulize kufanya utafiti kuhusu jinsi mapato yanapeanwa. Kisha kulingana na utafiti, eleza ni kwa nini wanahitaji nyongeza ya mapato yao na saidia maombi yao ukitumia maelezo na ukweli.
- Zungumza kuhusu taarifa pamoja. Chagua hadithi moja, isome na mtoto wako na mjadiliane maana yake.
- Zungumza na mtoto wako kuhusu lengo lao. Wanataka kufanya nini wakimaliza sekondari? Sikiliza wanavyosema na uwape mawaidha ili kusaidia kufikia malengo yao.

## **Ni nini mwanafunzi wako anapaswa kujua na kuweza kufanya katika sanaa ya lugha ya kiingereza (ELA):**

### **Lugha**

- Elewa lugha ya mfano (lugha ya kujieleza ukitumia maneno yaliyoko nje ya maana ya awali). Kwa mfano: “Jua linang’aa kama almasi katika uso wa maji.”
- Tumia mahojiano kukusanya habari za utafiti wa mradi, kama vile historia ya familia.
- Elewa hila tofauti ya maana kulingana na maneno, kama vile baridi.
- Jenga ufahamu wa elimu ya maneno ukitilia mkazo yale yaliyo na lengo la kutofautisha mawazo ama uhusiano, kama vile “kwa upande mwingine”, “vile vile”, na “kwa hiyo”.
- Onyesha umaarufu wa mikataba ya lugha ya kiingereza – herufi kubwa, alama, na maneno.

### **Kusoma na Fasihi**

- Tofautisha na uchambue
  - Mawazo makuu, makala ya maandishi, na maelezo ya kusaidia katika vitabu vya hadithi ama jarida.
  - Jinsi mwandishi anatumia mazungumzo na maelezo katika kitabu cha hadithi au hadithi.
  - Jinsi mwandishi anatumia kikao, tabia za wahusika, na njama katika hadithi na vitabu.
- Uganisha habari kutoka sehemu tofauti za chanzo za magazeti ama digitali kujibu maswali na kutatua matatizo.

### **Kuandika**

- Chambua fasihi na jarida na uandike kipande ambacho kikopamoja na maelezo kutoka kwa maneno ya kusaidia. Kwa mfano: andika barua kwa mwandishi ama kwa kampuni.
- Andika ripoti ya utafiti ukitumia maneno yao, lengo sahihi na maelezo ya kusaidia.
- Andika hadithi za mwanzo ambazo zina mambo ya kawaida ya kutunga: njama, wahusika, na kikao na uongeze mazungumzo, maelezo, na ufanisi wa kuharakisha tukio.
- Andika maoni ambayo yanapeana ukweli na mifano ambayo imeunganishwa pamoja kusaidia msimamo wa mwandishi.



## Jinsi ya Kuhimiza Masomo ya ELA Nyumbani

- Jadiliana kuhusu historia ya familia yako na mtoto wako. Himiza mtoto wako kufikiri juu ya maswali, kuhoji familia, na kutengeneza kitabu cha picha akitumia hadithi hizo pamoja na picha za jamaa na mababu.
  - Soma kwa sauti sura ya kitabu pamoja na mtoto wako kila siku. Jadili njama na wahusika. Uliza maswali. Kwa mfano: "Kuna migogoro gani katika hadithi?" "Mhusika mkuu anabadilika vipi na kwa nini?" Linganisha na maisha yenu na vitabu vingine ambavyo mmevisoma pamoja.
  - Tembelea maeno ya kihistoria, kama vile Freedom Trail at Raven Run ama MacAdam Student Observatory katika Chuo Kikuu cha Kentucky, pamoja na mtoto wako. Chagua biografia katika maktaba ya umma kuhusu wenyeji maarufu wa kata ya Fayette. Zungumza na mtoto wako kuhusu vile maeno ya kihistoria yanafanya hadithi kuwa kweli na jinsi mijengo inaonekana ya kuvutia sana na muhimu.

*Tafadhalii ungana na mwalimu wa mtoto wako na uulize kuhusu rasilimali za masomo ya nyumbani zinazohusika na programu za kipekee za kusoma na kuandika.*

## **Ni nini mwanafunzi wako anatakiwa kujua na kuweza kufanya katika hesabu:**

- Suluhisha hesabu katika kuongeza, kuondoa, kuzidisha, na kuganwanya ukitumia nambari kubwa na hesabu za hatua nyingi.
- Elewa uhusuno baina ya fraksheni, nukta na asilima.
- Fafanua mfumo wa thamani iwe pamoja na nukta, na kuhesabu na nukta kufikia mamia (sehemu mbili kutoka kwa nukta).
- Ongeza na kuondoa fraksheni pamoja na denimineta zisizo sawa (Nambari ya chini ya fraksheni) na suluhisha hesabu za maneo ya aina hii. Kwa mfano:  $2\frac{1}{4} - 1\frac{1}{3}$ .
- Zidisha fraksheni; gawanya fraksheni katika sehemu rahisi; na suluhisha hesabu zinazohusiana. Kwa mfano: Tafuta eneo la rectango iliyio na fraksheni ya urefu kwa upande; ama kama watu 3 wanashiriki  $\frac{1}{2}$  paundi ya chocolate kisawa.
- Elewa maana ya kiasi, na usuluhishe hesabu za maneno ambazo zinahusiana na kiasi.
- Wasilisha na utafsiri uhusiano baina ya vitu viwili tofauti, kama vile muda na urefu. Kwa mfano: chora msitari wa grafu ya jinsi mtu amekua kati ya miaka 2 na 10 na chambua ni lini ukuaji unatokea katika kiwango kikubwa ama kidogo.
- Elewa kwamba pembe nne zinaweza kuwekwa kwa kundi zaidi ya moja. Pembe nne ni kitu chochote cha kona nne, kama vile msambamba na trapezoidi.
- Tafuta kisai na sehemu ya uso wa rektangyula prisms. Rectangyula prism ni kitu chenye pembe tatu ambacho kina nyuso sita ambazo ziko kama rektango kama boksi ya viatu.



## Jinsi ya Kuhimiza Mafunzo ya Hesabu Nyumbani

- Wacha mtot wako apime urefu wa pande za chumba katika nyumba yako na kisha akadirie mviringo na eneo la chumba. Mtoto wako anaweza pia kipima chumba tofauti na kulinganisha miviringo na eneo la vyumba hivyo viwili.
  - Tafuta fursa kila siku kutumia nambari kubwa pamoja na mtoto wako. Kwa mfano: linganisha bei ya modeli tofauti za magari yalijotangazwa katika magazeti ama linganisha umati wa Lexington na umati wa mji wa jamaa ama rafiki.
  - Tafuta fraksheni na asilimia katika mauzo katika maduka ya mtaani. Ambia mtoto wako afikirie ni pesa ngapi unaweza kuokoa katika kila kile ununuacho.
  - Ongeza na kuondoa dola na mapeni ukitumia nukta katika maisha ya kila siku. Ambia mtoto wako kwanza akadirie bei ya vitu vitatu ama zaidi kisha ajumuushe.

*Tafadhali ungana na mwalimu wa mtoto wako na uuilize kuhusu rasilimali za masomo ya nyumbani zinazohusika na programu za kipekee za hesabu.*

**FAYETTE COUNTY PUBLIC SCHOOLS**

1126 Russell Cave Road  
Lexington, KY 40505

859-381-4100  
[www.fcps.net](http://www.fcps.net)

*Hii brosha ilichapishwa na Shule za Umma za Kata ya Fayette.*

*Ilitengenezwa Fall 2016*